# MAONI YA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (LHRC) KUHUSU MABORESHO YA MFUMO WA HAKI JINAI KWA TUME YA RAIS YA MABORESHO YA MFUMO WA HAKI JINAI NCHINI

## INAYOONGOZWA NA JAJI MKUU MSTAAFU MHE. MOHAMED OTHUMAN CHANDE

**Imewasilishwa Februari 20, 2023 Na;**

**Anna Henga (Wakili)**

**Mkurugenzi Wa Kituo Cha Sheria Na Haki Za Binadamu (LHRC)**

## A. UTANGULIZI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni shirika lisilokuwa la kiserikali, lisilogawana faida lenye lengo la kujenga uwezo kwa umma kuhusu Haki za Binadamu, kukuza na kulinda Haki za Binadamu na Utawala bora nchini.

LHRC imefanya shughuli mbalimbali za kiuchechemuzi ili kuchagiza maboresho ya sheria za haki jinai, shughuli hizo zilihusisha mikutano na mawaziri mbalimbali, makatibu na manaibu wa wizara, pamoja na wakuu wa idara mbalimbali wa sheria kwa vipindi tofauti vya uongozi.

Kwa upande mwingine, LHRC imefanya mikutano ya kimkakati na kamati mbalimbali za bunge ili kuonyesha ukubwa wa tatizo kufuatia malalamiko na kesi tulizofanya katika programu za kutoa msaada wa kisheria katika mikoa yote nchini. LHRC pia imefanya juhudi za makusudi katika kujumuisha jinsia katika sekta mbalimbali ili kuhakikisha mahitaji ya wanawake na watu wenye ulemavu yanasimamiwa ipasavyo kwa kuendelea kutoa elimu na mafunzo mbalimbali ya uzingatiaji jinsia katika utekelezaji kwenye haki jinai hasa watoto na wanawake.

Hata hivyo, mbali na shughuli za mikutano, Kituo kimetoa mchango wake pale ilipohitajika na mara nyingine kwa jitihada binafsi kwa kutoa maoni mbele ya Kamati za Bunge kuhusu mabadiliko ya sheria za jinai. Kwa kutambua haki za binadamu, Kituo kiliungana na wadau wengine kuandika sheria ya mfano ya Msaada wa Sheria ambayo kwa kiasi kikubwa imepelekea kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Sheria, 2017.

Kwa mwaka, 2022 Kituo kiliandaa Muswada wa mfano ya Kuanzisha Chombo Maalum cha Kusimamia Mwenendo wa Jeshi la Polisi, *(Kiambatanisho namba 2)* ikiwa ni sehemu ya mchano wake katika jitihada za kuboresha mfumo wa utoaji haki jinai nchini. Vikao mbalimbali vilifanyika kwa mwaka 2022 chini ya uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa ajili ya kuijadili na kuona namna bora ya kusimamia na kuboresha mfumo wa kisheria wa kusimamia mwenendo wa Jeshi la Polisi.

Kwa upande mwingine, LHRC imefanya jitihada za uchechemuzi wa kutungwa kwa Mpango wa Taifa wa Haki za Binadamu wa awamu ya pili ambao bado uko kwenye rasimu, hivyo tunatoa wito kwa Tume hii kuweka kipaumbele mapendekezo ya kutungwa na kutekelezwa kwa mpango huo.

## B. KUHUSU MAPENDEKEZO

LHRC inaleta mapendekezo yake juu ya maoni ya maboresho ya taasisi za haki jinai yatakayopelekea kuboreshwa kwa mfumo wa Haki Jinai. LHRC imepokea kwa furaha wito huo kwa kuwa Kituo kimetamani kuwa na maboresho haya kwa muda mrefu.

Mapendekezo ya Kituo yametokana na uchambuzi wa malalamiko tuliyoyapokea, kesi wakati wa kutoa msaada wa sheria na uchambuzi wa sheria na mikataba mbalimbali ya kimataifa ya haki za binadamu.

**I. Baadhi ya mikataba ya Kimataifa hii ni kama vile;**

i. Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu, 1948.
ii. Mkataba wa Haki za Kiraia na Kisiasa, 1966.
iii. Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto, 1989.
iv. Mkataba wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake,1979.
v. Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu, 2006,
vi. Mkataba wa nyongeza wa Afrika wa Haki za wanawake (Maputo Protocol), 2003.
vii. Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, 1981.
viii. Mkataba wa Afrika Ustawi wa Mtoto, 1990.
ix. Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Wafungwa, 1949.
x. Kanuni za Tokyo na Bangkok, 1963.
xi. Tamko la Vienna la Haki Jinai, 2000.

**II. Sheria za Ndani**

i. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.
ii. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985.
iii. Sheria ya Ofisi ya Mashataka ya Taifa, 2008 R.E 2002.
iv. Sheria ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, 1984 R.E.
v. Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi,
vi. Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya, 2016 R.E 2002.
vii. Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji Fedha, Sura Namba 423 R.E 2022.

viii. Sheria Utawala wa Mahakama, 2011.
ix. Sheria ya Kuchunguza Vifo, 1980.
x. Sheria ya Bodi za Parole, 1998 Sura Namba 400.
xi. Sheria ya Kupambana na Kudhibiti Rushwa, 2007 R.E 2022.
xii. Sheria ya Mazao ya Jinai, Sura 256 R.E 2002.

**III. Tafiti, Taarifa na Maamuzi ya Mahakama Kuu na Rufani**

i. Taarifa ya Haki za Binadamu, 2021.
ii. Taarifa Maalum ya utafiti wa nchi tano (5) kuhusu makosa yasiyokuwa na dhamana, 2021.
iii. TaarifaUfanisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, 2022.
iv. Kesi ya Maneno Rashid dhidi ya Jamhuri, Rufaa namba 11 ya 2021.

## C. MUUNDO WA MAPENDEKEZO

**Mapendekezo yamegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni;**

I. Mapendekezo ya jumla
II. Mapendekezo mahususi

## MAPENDEKEZO YA JUMLA

**Wito: Kufumuliwa kwa Sheria yote ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985, Sheria ya Ushahidi na Kanuni ya Adhabu, Sura 16.**

**1. Changamoto za utendaji kazi wa Polisi**

**Maelezo :**

Japo sheria imeweka utaratibu mzuri wa namna ya ukamataji, bado kumekuwa wimbi la namna ya ukamataji wa watuhumiwa unaofanywa na baadhi ya maafisa wa Jeshi la Polisi ambao ni kinyume na sheria. Ukamataji huo umekuwa ukifanywa bila ya Afisa husika wa Polisi kujitambulisha , na mara nyingine bila sare za Jeshi la Polisi, bila magari rasmi ya polisi, ambayo mengine hayana namba za utambulisho au usajili wa gari hilo *“Plate number”*.

Suala la ukamataji wa watoto pia linaenda kinyume na sheria kwani watoto hawatakiwi kuoneshwa silaha na ukamataji hautakiwi kuwa wa nguvu. Lakini watoto wengi waliowahi kukamatwa na polisi wanakiri ukamataji huo ulivunja haki zao za msingi.

Pia wasimamamizi wa haki jinai wamekuwa wakitumia nafasi zao kusuluhisha makosa ya ukatili na hivyo kufanya kesi nyingi kuishia vituo vya polisi. Katika mafunzo ya waendesha mashtaka yaliyofanywa na LHRC 2022, ofisi ya DPP ilisema asilimia kubwa ya kesi zinazoripotiwa huishia polisi na chache tu hupelekwa mahakamani.

Kwa mara kadhaa, viongozi wakubwa wa nchi wamezungumzia kuwepo kwa kesi za kubambikizwa, wakielekeza lawama kwa Jeshi la Polisi. Yapo malalamiko ya wananchi pia kuhusu suala hilo. Licha ya malalamiko ya wananchi na maonyo ya viongozi, bado tatizo hili limeshika kasi.

a) Itakumbukwa Februari Mwaka 2020, aliyekuwa Rais wa awamu ya tano (5) Hayati John Pombe Magufuli alirusha lawama kwa vyombo vya dola na wapelelezi kuanzisha kesi zisizokuwa na msingi wala ushahidi inayopelekea kesi kuchukua muda mrefu.
b) Mwaka 2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan alieleza hisia zake juu ya uwepo wa kesi za kubambikiza na akatoa wito mwezi Mei, 2021 kwa aliyekuwa Inspekta Jenerali wa Polisi, Simon Sirro kufanya maboresho makubwa ya Jeshi la Polisi.
c) Mwezi Julai, 2021 aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani Mhe. George Simbachawene aliwataka Polisi kuacha tabia ya kubambikiza kesi.

Aidha Kumekuwa na tatizo la kimtazamo kati ya pande mbili tajwa, mathalani mara nyingi pale ofisa wa Polisi anamtazamo mtu aliyemkamata kama *“mhalifu”* badala ya kumtazama au kumchukulia kuwa ni mtuhumiwa.

Hali kadhalika, kwa upande wa wananchi ni ngumu kuwa katika mtazamo na uhalisia wa ofisa wa Polisi pale anapomkamata mtuhumiwa. Hii inaonesha kuna ombwe kubwa linalohitaji ufumbuzi na kuliziba.

Kwa upande mwingine, mahabusu wa kike kufanyishwa kazi katika vituo vya polisi.

**Mapendekezo:**

1. Kuundwa kwa Chombo Maalumu cha Kuangalia utendaji kazi wa Polisi
2. Kufumuliwa kwa mitaala ya mafunzo ya vyuo vya polisi.
3. Polisi wapewe elimu ya njia bora ya kushughulikia kesi za watoto wanaokinzana na sheria.Kuwekwa mfumo wa uwajibikaji kwa maafisa watakao bainika kubambikiza kesi. Tunashauri kutungwa kwa Sheria ya Police Oversight Board ilikukomesha suala hili.

4. Kuanzisha Progamu shirikishi za elimu kati ya Jeshi la Polisi na Wananchi kuhusu umuhimu wa Jeshi la Polisi na Wananchi katika kuboresha ulinzi na usalama, njia hii kupunguza mtazamo hasi na kurekebisha tabia za baadhi Polisi zinamtazama mtuhumiwa kama "*mhalifu*" na kwa upande wa wananchi wanaotazama polisi kama watesi na waonevu katika jamii.

## 2. Tatizo la usalama na ulinzi wa wanawake na Watoto

**Maelezo:**

Kumekuwa ongezeko la matukio ya mauaji, ukatili wa kingono na kimwili dhidi ya wanawake katika mikoa mbalimbali nchini yanayotokana na wivu wa mapenzi. Matukio haya yanahatarisha ulinzi na usalama wa wanawake . Matukio ya kuongezeka kwa vitendo vya Ukatili hasa wa kingono yamekuwa yakishamiri kila kukicha na kuitia serikali hasara ya kupambana na uhalifu huu. Kwa mujibu wa Taarifa ya Haki za Binadamu, 2021 imeeleza kuwa vitendo hivyo vinatokea katika ngazi ya familia.Taarifa ya Ofisi ya Umoja wa Mataifa Kudhibiti madawa ya Kulevya na Makosa ya Jinai (UNDOC), 2019 imetoa taarifa kukithiri kwa ukatili wa wenza unaopelekea mauaji, ambao umeendelea kuathiri zaidi wanawake

**Mapendekezo:**

Kituo kinapendekeza kuimarisha mfumo wa ustawi wa jamii kwa kuongeza uwezo kwa watumishi hao kuweza kusaidia utatuzi wa migogoro pamoja na ulinzi wa watoto katika jamii, kuweka mifumo ya usimamizi bora wa kesi za Ukatili na utoaji wa huduma ya baada ya Ukatili ili kujenga kizazi salama. Kujengea uwezo wataalamu wa haki jinai katika kutatua kesi za ukatili na kutoa huduma stahiki.Pia kituo kinaendelea kusisitiza kuhusu ushahidi hasa kwa kesi za ubakaji ambao unamtaka mtu kutoa taarifa baada ya kitendo tu, kwani suala hili limewanyima haki wahanga wengi, tunashauri serikali iboreshe upatikanaji wa ushahidi katika kesi za ubakaji. Ni asilimia ndogo ya wanaoweza kuripoti haraka iwezekanavyo kulingana na masuala ya miundombinu, uelewa na upatikanaji wa huduma.

## 3. Upelelezi wa kesi kuchukua muda mrefu

**Maelezo;**

Kwa mujibu wa taarifa ya Ufanisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kuhusu Mfumo wa Haki Jinai, ripoti imebainisha changamoto mbalimbali ikiwemo upelelezi kuchukua muda mrefu. Pamoja na ripoti hiyo, wapelelezi wa mikoa (RCO) na wawilaya (DCO) wameonekana kuwa na changamoto za kiutendaji. <u>*Katika kesi ya Mahakama Kuu kati ya Maneno Rashid dhidi ya Jamhuri, Rufaa namba 11, 2021.*</u>

Jaji Mwembe alisema " Mahakama hii na Mahakama ya Rufani mara kadhaa imelalamika na kukemea vitendo vya Jeshi la Polisi kufanya upelelezi au uchunguzi chini ya kiwango…"

Suala la ucheleweshaji wa kesi limeendelea kushamiri zaidi kwenye kesi za Ukatili ambapo hupelekea kukatisha tamaa wahanga na mashahidi na mwishowe kesi kufutwa na kuathiri upatikananji haki.

Suala la uchukuaji ushahidi kwenye kesi zinazohusisha watoto pia limekuwa likivunja haki zao kwani mara nyingi polisi hawasubirii uwepo wa maafisa ustawi au walezi na mtoto kuhojiwa peke yake.

**Mapendekezo**

1. Kuimarisha mifumo ya upelelezi ikiwemo kuweka ukomo.
2. Wasimamizi wa haki wazingatie haki za watoto katika kuchukua ushahidi kwa kufuata sheria, miongozo, kanuni na taratibu.
3. Kuweka bajeti stahiki kwa ajili ya upelelezi wa kesi ikiwemo kuhusisha matumizi ya teknolojia zaidi.

## 4. Kutotekelezwa kwa Maamuzi ya Mahakama

Mathalani, *Kifungu cha 148 (4)* kilitamkwa na Mahakama ya Rufani kuwa ni batili na kuwa kinyume cha sheria bado hakijafanyiwa marekebisho yoyote.

Aidha, kifungu kama hicho hicho kimeendelea kuwepo kwenye sheria nyingine kama vile kifungu *36 (2) cha Sheria ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa, Sura 200* na *Kifungu 19 cha Sheria ya Usalama wa Taifa, 1970 kinampa mamlaka Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuweka hati ya kuzuia dhamana kama ilivyokuwa awali katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985.*

**Rejea Kesi iliyofuta kifungu cha 148(4):**

*Kesi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Jeremiah Mtobesya, Rufaa Namba 65, 2016 Mahakama ya Rufani Tanzania, Dar es salaam mbele ya majaji B. M Luanda, K.M Mussa, B.M.K Mmilla, S.E Mugasha pamoja na J.C.M Mwambegele.*

**Mapendekezo**

1. Kurekebisha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinani, 1985 kwa kufuta kifungu cha 148(4).

2.Kufuta kifungu cha 36(2) na kifungu cha 19 cha Sheria ya Ulinzi wa Taifa, 1970 ili kuendana na principle ya *statute in pari materia, kuwa kama kifungu kimefutwa kwenye sheria moja basi kifungu hicho kinapaswa kufutwa kwenye sheria nyingine kwa kuwa vinamaana sawa.*

## 5. Utekelezaji wa mapendekezo ya Ripoti ya Jaji Nyalali

Tunaalika Tume hii ya Rais, ijiongoze kwenye mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Jaji Francis Nyalali, kuhusu sheria arobaini (40) ambazo hadi sasa takribani miaka ishirini (20) mapendekezo yake hajatekelezwa kwa kiasi kikubwa. Rejea kiambatanisho namba 6 yenye Taarifa ya LHRC kuhusu utekelezaji wa Mapendekezo ya Ripoti ya Jaji Francis Nyalali.

## 6. Kupunguza mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka wa Serikali (DPP)

**Maelezo**

Sheria iweke vigezo maalumu vitakavyoiongoza mahakama katika kufikia uamuzi wa kutoa au kutooa dhamana katika makosa yasikuwa na dhamana, badala ya kumpa mamlaka makubwa DPP. Kama ilivyo nchini Kenya, na baadhi ya nchi kama vilie Uganda, Malawi na Zambia zilivyoweka utaratibu maalum wa kushughulikia makosa yasiyokuwa na dhamana.

Tume irejee katika *Kiambatanisho namba 4.*

**Mapendekezo:**

Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Uhujumu Uchumi zifanyiwe marekebisho kwa kuipatia mahakama uwezo wa kupokea na kusikiliza dhamana katika makosa yasiyokuwa na dhamana pasipo kuwa na mamlaka ya upande mmoja wa DPP kuweka hati ya kuzuia dhamana.

## 7. Kuboreshwa kwa miundombinu ili kukidhi mahitaji ya kijinsia;

- Kuweka mikakati ya kukidhi mahitaji ya wafungwa wanaonyonyesha na wenye mahitaji maalum.
- Kuhakikisha mahakama, polisi pamoja na magereza wana mahitaji ya muhimu kwa watu wenye ulemavu ikiwemo huduma ya lugha ya alama, ufikiwaji na upatikanaji wa huduma za msaada. Mtu mwenye ulemavu anapokuwa mahabusu ni ngumu kwenda na msaidizi wake hivyo huduma zinatakiwa kuboreshwa.

- Kutoa njia mbadala kwa wanawake wanyonyeshao na wajawazito wanaokuwa mahabusu kwani wanashindwa kutoa huduma stahiki kwa watoto ambao hawana hatia. Ikumbukwe mwaka 2022 mwanamke mjamzito alifariki katika Kituo cha Polisi.
- Kutoa huduma mbadala za watoto wanaoingiliana na sheria ili waweze kufurahia utoto wao pale mama wanapohukumiwa kwenda gerezani
- Kuboresha huduma katika magereza za wanawake kwa kuhakikisha kunakuwa na bajeti ya kuwapa huduma za kijinsia kama za hedhi salama na nyinginezo.
- Kuboresha mazingira ya magereza za wanawake ili kuhakikisha usalama wa Afya zao kwani mara nyingi wanawake kutokana na maumbile yao ni rahisi kupata magonjwa mbalimbali.
- Kuhakikisha mahakama za watoto zinaimarishwa hasa zile za wilaya ambazo ziliteuliwa na Jaji mkuu kuweza kupambana na tatizo la upunguzfu wa mahakama za watoto. Mahakama hizo hazina vigezo vya kuwa mahakama za watoto na hivyo serikali ifanye juhudi kuziimarisha kuweza kufikia vigezo.
- Uwakilishi kwa watoto wanaokinzana na sheria kwani wengi hujiwakilisha wennyewe na hivyo kutokuwa na uwiano katika uendeshaji kesi zao. Serikali yaweza fanya hivi kwa kutumia chama cha mawakili kama probono.

## 8.Kufuta Adhabu ya Kifo (Mandatory Death Penalty) kwa kurekebisha Kifungu cha 39, 40 na 197 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura Namba 16

**Maelezo ya suala:**

Adhabu ya kifo ni adhabu inayotweza utu wa mtu na kuvunja haki ya kuishi kama ilivyoainishwa katika Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ya Haki za Binadamu.

Aidha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na watu katika shauri la ***Ally Rajabu na wenzie dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Shauri Namba 007/2015*** katiba uamuzi wake uliotolewa Novemba 2019 ilisema adhabu ya kifo ya lazima inakiuka Haki za Binadamu na Tanzania ikaamuriwa ifute adhabu hiyo lakini mpaka leo uamuzi haujatekelezwa.

Pia, mwaka 1992 Ripoti ya Tume ya Jaji Nyalali; ilitoa mapendekezo ya kufanya marekebisho ya sheria ili kuondoa adhabu ya kifo kwa kuwa ni ya kikoloni na isiyo ya kibinadamu. Pamoja na mapendekezo hayo hadi sasa bado hakuna utekelezaji wake.

**Mapendekezo**

Kurekebisha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 kwa kufuta au kutoa ulazima wa mahakama kutoa adhabu hiyo.

## 9.Kuimarisha mifumo ya kisheria, sera na mienendo ya vyombo vya dola

**Maelezo:**

Licha ya *ibara ya 147(3) ya Katiba* ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 kukataza majeshi yetu ikiwemo Jeshi la Polisi kujihusisha na shughuli za kisiasa, bado kuna changamoto ya utekelezaji wa ibara hiyo. Kwa mfano; mwaka 2019, aliyekuwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Arusha Jonathan Shana alisikika akitumia salamu ya "Kidumu Chama cha Mapinduzi alitoa kauli hiyo Butiama mkoani Mara wakati wa hafla ya kumbukizi ya miaka 19 ya Kifo cha Baba wa Taifa, huku akisisitza angependa vyama vingine vife.

Pia, aliyekuwa Kamanda wa Polisi Wilaya ya Hai Lwelwe Mpina alikuwa anajibizana na Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuwa asingeweza kushinda uchaguzi. Hii inalipunguzia uhalali wa Jeshi la Polisi hasa linapombana na tuhuma za uhalifu unaohusisha mambo ya kisiasa.

**Mapendekezo:**

Kuimarisha mifumo ya kisheria, kisera na mienendo ya vyombo vya dola.

## 10. Kuundwa kwa Chombo Huru cha Kusimamia Mwenendo wa Polisi

## 11. Kuondoa gharama za ukamataji na usafirishaji wa watuhumiwa kwa wahusika wa kesi

# MAPENDEKEZO MAHUSUSI

| 1. | ELEZA MAMBO AU MAENEO YANAYOHUSU HAKI JINAI UNAYOYAJUA AMBAYO WANANCHI NA WADAU WENGINE WANAYALALAMIKIA KUHUSU HAKI JINAI KATIKA MFUMO NA MNYORORO MZIMA WA HAKI JINAI NCHINI. | | |
|---|---|---|---|
| | **Suala** | **Tatizo** | **Mapendekezo** |
| 1. | Rushwa na haki ya dhamana | Pamoja na kuwepo kwa sheria inayotoa haki ya dhamana, bado kumekuwa na tatizo kubwa la mtuhumiwa wa kosa la jinai kupata dhamana akiwa mikonomi mwa Polisi.<br><br>Kwa mujibu wa Ripoti ya Haki za Binadamu, 2021 ;<br>Wananchi walitoa maoni yao juu ya ukubwa wa tatizo la kupata dhamana, asilimia 46% walisema upatikanaji wa dhamana ni tatizo, asilimia 35% walisema upatikanaji wa dhamana ni tatizo kubwa sana, asilimia 16% walisema dhamana ni tatizo la kawaida, wakati asilimia 1% walisema dhamana si tatizo.<br><br>Matokeo ya utafiti yanaonesha wazi kuwa upatikanaji wa dhamana ya Polisi ni tatizo katika jamii yetu.<br><br>Kiini cha tatizo hili linaambatana na haki ya dhamana kutumika kama mtaji wa wapelelezi wa kesi fulani, hivyo humng'ang'ania mtuhumiwa | Kuwe na mfumo wa wazi wa utoaji wa dhamana, mathalani kuanza kutumia teknolojia ili kuomba dhamana, hii itaweka uwazi wa mtu au mahali ambapo ombi la dhamana lilipokwama au kufikia.<br><br>Pia jitihada za makusudi zinapaswa kuchukuliwa kudhibiti kabisa mianya ya rushwa katika vituo vya Polisi.<br><br>**Msingi:**<br>Na itaendelea kuvunja *Ibara ya 13 (6) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.* |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kwa kuweka mazingira magumu ili mtu huyu asipewe dhamana bila kujiongeza kwa kutafuta namna ya upendeleo kwa kutoa rushwa.<br><br>Tatizo la rushwa limeendelea kuwa sugu katika vituo vingi vya Polisi hapa nchini. | |
| 2. | Ukamataji na Upekuzi | 1. Ukamataji na Upekuzi usiyofuata sheria umesababisha kuibuka kwa vikundi vya kihalifu ambavyo wananchi wanashindwa kutofautisha kuwa ni Polisi au ni watu wahalifu. Mathalani ukamataji wa **Tito Elias Magoti** ulikuwa ni kinyume kabisa na sheria, Tito angeweza kuitwa au kukamatwa akiwa kazini kwake Kijitonyama, badala yake alitekwa na kutoonekana kwa zaidi ya siku mbili na taarifa zake hazikupatikana katika kituo chochote cha Polisi.<br>2. Ukamataji wa watoto uzingatie sheria na mikataba ikiwemo kutoonesha silaha kwa watoto wanaokinzana na sheria<br>3. | 1. Kuboreshwa kwa mifumo ya mafunzo na mitaala ya Jeshi la Polisi.<br>2. Jeshi la Polisi kutoa taarifa sahihi kwa uharaka ikiwa kuna ukamataji<br>3. kama utekaji na kutoa ufafanuzi kwa umma.<br><br>**Msingi:** Kuendana na *Ibara ya 9 (2) ya Mkataba wa Kisiasa na Kiraia, 1966* unaoweka hitaji la mtu anayekamatwa kupewa sababu za kukamatwa kwake. |
| 3. | Kukamata wazururaji | Kwa mujibu wa *Kifungu cha 16* cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinaruhusu mtu yoyote | Kurekebisha kwa kufuata kosa hilo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kumkamata mzururaji pasipo kuweka utaratibu baada ya kumkamata.<br><br>Pia, kutokana na ugumu wa maisha na ukosefu wa kazi, kuna uwezekano mkubwa wa watu wengi wakaingia hatiani kwa sheria hii, endapo ikitekelezwa kama ilivyo.<br><br>Kwa eneo la Dar Es Salaam, vijana wengi wanaokamatwa kwa 'kosa' hilo, hufikishwa Mahakama ya Jiji, wengi hukubali kosa na kufungwa siku 14 jela.<br>Kutoruhusu wakamatwaji kutoa taarifa kwa ndugu zao na hivyo kukaa mahabusu au polisi kwa muda mrefu kwa makosa yenye dhamana. | **Msingi:** Inapingana na haki ya kuwa huru kwa mujibu wa *Ibara ya 3 ya Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu, 1948, Ibara ya 9 ya Mkataba wa Haki za Kiraia na Kisiasa, 1966 na Ibara ya 6 ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, 1981.* |
| 4. | Mfumo wa *Parole* | Udhaifu wa bodi za parole za mikoa na ile ya Taifa, muundo wake hauakisi uhalisia.<br>Huduma hii pia iwe kipaumbele kwa wanawake wenye watoto na wajawazito ili kuwalinda watoto kulingana na utaratibu utakaowekwa. | Kituo kinapendekeza kuimarishwa kwa bodi za parole za mikoa na ile ya Taifa ili kuweza kuongeza ufanisi wa bodi hizo hususani muundo wa bodi ili kuongeza wigo wa wajumbe wa bodi hizo ikiwepo, Ustawi wa Jamii na Asasi za Kiraia. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Huduma hii pia iwe kipaumbele kwa watu wenye ulemavu kulingana na uataratibu utakaowekwa. | |
| 5. | Kufuta Committal Proceeding | Watuhumiwa kukaa muda mrefu kwenye mahakama ambayo kimsingi haina mamlaka ya kusikiliza shauri husika.<br>Kwa mfano tunayo mifano ya watuhumiwa waliokaa mahabusu miaka mitano kwa sababu tu mashauri yao yalikuwa katika ngazi ya *committal* kuna sababu gani ya kumpeleka mtuhumiwa kwenye mahakama ambayo kimsingi haina mamlaka ya kusikiliza shauri husika. | Kituo kinapendekeza kufutwa kwa takwa la kuwa na commital kwenye mashauri ya uhujumu uchumi. |
| 6. | Baadhi ya mamlaka zisizo Jeshi la Polisi kupewa mamlaka ya Polisi ukamataji, upekuzi na uchunguzi | Miaka ya hivi karibuni iliibuka kasumba ya baadhi ya taasisi zisizo jeshi la Polisi kupewa mamlaka ya Kipolisi<br><br>Mfano wa taasisi hizo ni TAKUKURU, Mamlaka ya Madawa ya kulevya, TRA, Idara ya Kudhibiti Fedha Haramu (FIU) na taasisi nyinginezo zinazofanana na hizo. | Kituo kinapendekeza kufanyika kwa marekebisho ya sheria ili kufungamanisha majukumu ya ukamataji na upekuzi kubakia kwenye jeshi la Polisi pekee.<br><br>Kufungamanishwa kwa taasisi zote zinazojihusis na jinai nchini ili majukumu ya ukamataji na umiliki wa mahabusu libaki kuwa jukumu la jeshi la Polisi pekee tofauti na miaka ya hivi karibuni kila taasisi au mamlaka inayojihusisha ama moja kwa moja au vinginevyo na haki jinai kuwa na majukumu ya Polisi kumiliki mahabusu. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Hii itasaidia kupunguza malalamiko ya watanzania kutekwa na kukamatwa na watu wasiokuwa na sare za jeshi la Polisi, malalamiko ambayo tumekuwa tukiyapokea kwa mda mrefu.<br><br>Tunapendekeza taasisi tajwa zinapotaka kufanya oparesheni zake ziombe msaada wa jeshi la Polisi na sio kujivika majukumu ambayo hazina kisheria. |
| 7. | Mfumo wa uwajibikaji wa maofisa wa Polisi | Kumekuwa na vitendo vya uonevu dhidi ya wananchi vinavyofanywa na baadhi ya maofisa wa Polisi, mfumo wa ndani wa uwajibishaji hauna uwazi unaoweza kuthibitisha na kuridhisha jamii kuwa ofisa aliyetenda kosa hilo nayeye amewajibishwa. | Kuwa na chombo maalam cha kuwajibisha maofisa wa Polisi wataokiuka maadili pamoja na sheria.<br>Serikali ihakikisha Jeshi la polisi lina bajeti stahiki ili kuacha kuweka mzigo kwa nwatuhumiwa na familia zao au wahusika kwenye kesi kwani hupeleka haki kuingiliwa. |
| 8. | Kutotolewa kwa taaarifa za ripoti za uchunguzi | Taarifa mbalimbali za kiupelelezi/uchunguzi kutotolewa kwa wakati, au kutojitosheleza au kutotolewa kabisa.<br>Mathalani tukio la kutekwa kwa mfanyabiashara maarufu “Mo Dewji” ilipekea hadi Rais wa Awamu ya Tano kuhoji **hadharani juu ya utata wa taarifa hiyo.** Hii inamaana ya kwamba, taarifa hiyo haikujitosheleza. Pia, taarifa ya kupotea kwa vijana watano (5) kwa | Kutolewa kwa taarifa za kiuchunguzi ili umma uweze kujua. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | majina; **Tawfiq Mohamed, Seif Swala, Edwin Kunambi, Hemed Abass and Rajabu Mdoe** katika mazingira ya utata hadi leo hatma ya upatikanaji wao bado haijafikia mwisho. | |
| 9. | Mamlaka ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuweka watu vizuizini/korokoroni. | Wakuu wa Wilaya na Mikoa wamekuwa wakitumia vibaya Sheria ya Tawala za Mikoa, 1997 kwa kuamuru Jeshi la Polisi kumkamata mtu kwa lengo la kulinda usalama na amani katika eneo husika aidha mkoa au wilaya.<br><br>Hii hupelekea watu kuhukumiwa pasipo kusikilizwa kwa utaratibu mzuri wa kimahakama.<br>Pamoja na kelele za muda mrefu kutoka kwa wananchi juu ya matumizi ya mamlaka ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya bado sheria hii imeendelea kuwepo na kutumika. | Kufuta sheria hii,<br><br>**Msingi:**<br>Maamuzi ya Makahama Kuu Masjala ya Moshi Kesi ya Madai Namba 4, 2020 chini ya Jaji L.M Mlacha kati ya **Mary Peter Otaru (Mlalamikaji ) dhidi ya Onesmo Buswelu (Mdaawa namba 1 Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Moshi), Namsemba Mwakatobe (Mdaawa namba 2) na Mwanasheria wa Seriakali (Mdaawa namba** 3).<br><br>Mahakama Kuu iliamua ifuatavyo;<br>1. Kwamba, amri ya ukamataji na kutia kololoni kwa mlalamikaji uliofanywa na Mkuu wa Wilaya ulikuwa kinyume cha sheria.<br>2. Kwamba, mlalamikaji alipwe fidia ya jumla kiasi cha Tsh.Milioni 90, na fidia maalum Tsh.Milioni 10.<br>3. Kwamba, kiasi cha Tsh.Milioni 10 kitalipwa na Mkuu wa Wilaya, alafu kiasi kilichobaki cha Tsh.Milioni 90 italipwa na Serikali. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Hii inaonesha kuwa haki mtu huyo alionewa na Mkuu wa Wilaya, lakini pia Serikali imeingia hasara kwa sheria hii.<br><br>SHERIA HII IMEINGIZA HASARA NA MZIGO KWA WANANCHI KWAKUWA JUMLA YA TSH.MILIONI 90 ITALIPWA KUTOKA KATIKA KODI ZA WANANCHI.<br><br>Pia, maamuzi ya Mahakama ya Rufaa Tanzania mbele ya Jaji Nyalali kati ya Hatib Gandhi na Mwingine dhidi ya Jamhuri, 1996 Law Report page 12<br><br>“Hii siyo Jamhuri ya ndizi inayoendeshwa bila mifumo inayoendeshwa bila kuheshimu mifumo ya Kitaifa na Kimataifa. Kwamba ni nchi ambayo waliyopo madarakani wanafanya mambo pasipo kuheshimu sheria, watu wote wanaoshikiria ofisi za umma, lazima waongozwe na Katiba, Sheria na Kanuni zinazoongoza majukumu yao.<br><br>Lazima wakumbuke viapo vyao na wajibu wao kwa mujibu wa sheria, na Mahakama kama Muhimili wa tatu, unajukumu la kulinda na kuhifadhi katika na Sheria. |
| 10. | Tatizo la kubambikia kesi | 1. Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwa watu kubambikiwa kesi kwa mfano itakumbukwa mnamo mwezi Mei, 2021 Rais wa | 1. Kuweka mfumo wa uwajibikaji kwa wahusika pale endapo mahakama itathibitisha pasipo shaka kuwa kulikuwa na uonevu, usingiziwaji au ubambikiziaji wa kesi wa makusudi, hii itapunguza machungu ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo ya kufuta kesi zote za kubambikizwa ambapo jumla ya kesi 147 zilifutwa, mara nyingi kesi hubambikwa ili ili kufanikisha jambo fulani la kisiasa au kuzima agenda inayoshikiliwa kidedea katika jamii.<br>2. Kesi za watoto: Kubambikiziwa kesi na kusingiziwa umri.<br><br>Pia, kijana aitwaye Said Njwete aliyefananishwa na mtu aitwaye maarufu "Scorpion" alikamatwa na kuhumiwa na Mahakama ya Wilaya ya Ilala kifungo cha miaka 7 na kulipa faini ya shilingi milioni 30 kwa hatia ya kuumi kwa kumtoboa macho Bwana Said Mrisho mwaka 2018.<br><br>Kijana huyo aliachiwa huru na Mahakama ya Rufaa baada ya kubatilisha hukumu yake. | mtu aliyebambikiziwa kesi na kumrudisha katika hali yake ya mwanzoni ya kiuchumi, kijamii au kisiasa.<br><br>Pia,Kuimarisha ufikiwaji wa nafuu zilizopo – effective remedies, |
| 11. | Weledi mdogo katika kutathimini ushahidi. | Maamuzi ya mahakama ya rufani yanaonesha kwamba kumekuwa na weledi mdogo katika kutathimini ushahidi kabla kesi haijapelekwa | Kituo kinapendekeza kuimarishwa kwa ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa makosa ya jinai ili kuifanya ofisi hii muhimu kuwa na ufanisi wa kuchambua ushahidi kwa weledi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | mahakamani. Watuhumiwa wengi wametiwa hatiani kwa ushahidi ambao baadae huja kubatilishwa na mahakama za juu.<br><br>Kwa mfano katika kesi ya **Freeman Mbowe na wengine dhidi ya Jamhuri, Rufaa No. 76 ya 2020 iliyotokana na kesi ya jinai No. 112 ya 2018** katika mahakama ya hakimu mkazi kisutu mbele ya **Mhe T.k Simba, Mahakama kuu masijala ya Dar Es Salaam mbele ya Jaji I.C. MGETA** ilibatilisha hukumu ya mahakama ya kisutu kwa hoja kwamba hapakuwa na ushahidi wa kutosha uliowezesha kuwatia hatiani watuhumiwa. | Kama vile kupitia sera, mitaala na miongozo ya mafunzo ya upelelezi na uchunguzi ili kuendana na mazingira. |
| 12. | Kukosekana kwa dawati la jinsia katika baadhi ya vituo vya Polisi hasa vya vijijini na wilaya za mbali. Tunaipongeza serikali kwa kufikisha vituo 420 ila kuna uhitaji mkubwa bado. | 1.Kuna baadhi ya wahanga wa ukatili wa jinsia wakifika vituo vya Polisi wanashindwa kusikilizwa malalamiko yao kutokana na kutokuwa na dawati la jinsia katika vituo hivyo.<br>2. Baadhi ya maofisa katika dawati la jinsia katika vituo vya Polisi hutoa kauli mbaya haswa kwa wahanga wa jinsi ya kiume waliopitia vitendo vya ukatili wa kijinsia. | 1. Maofisa wa Polisi wanaofanya kazi katika dawati la jinsia kupewa mafunzo ya mara kwa mara ya kuhusu jinsia, pia kuwapa vipaumbele wale wenye umahiri wa elimu ya jinsia katika kazi za madawati ya jinsia, mfano wenye Diploma na Shahada na zaidi ili kuongeza ufanisi katika eneo hiyo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13. | Vitendo vya ukatili vinavifanywa na maafisa Polisi dhidi ya wananchi. | Baadhi ya maafisa Polisi wamekuwa wakifanya vitendo vya ukatili dhidi ya wananchi kama vile kuwateka na kuwapiga.<br><br>Na pia wamekuwa wakiwatuhumu pasipo kuwafungulia mashtaka yoyote, hii hufanya watuhumiwa kuteseka katika vituo vya polisi na mahabusu pasipo kufikishwa mahakamani kwa ajili ya kusikilizwa na kuamuliwa | Kuwe na chombo maalumu kitakacho wawajibisha maafisa Polisi ambao watakiuka sheria.<br><br>Rejea: Mafano mzuri katika nchi ya Kenya, na kiambatisho nambatanisho namba 2 cha Muswada wa Mfano wa Chombo hicho. |
| | Uwezo mdogo wa maafisa wa polisi kufanya uchunguzi wa kesi za jinai | Mahakama kuu ya Tanzania masijala ya Morogoro katika kesi ya Maneno Rashid Dhidi ya Jamhuri Rufaa No. 11. 2021 Mhe jaji Ngwembe katika ukurasa wa 10, 11 na 12 alikuwa na haya ya kusema, nanukuu;<br>"*Mahakama hii pamoja na Mahakama ya Rufani imekuwa ikilalamika juu ya ongezeko kubwa la jeshi la polisi kufanya uchunguzi wa hovyo, makosa ya ubakaji ni makosa makubwa katika nchi yetu yanayoweza kumtia hatiani mtu kwa adhabu ya miaka 30 hadi kifungo cha maisha. Hivyo kila mtu anayehusika katika upelelezi lazima atimize wajibu wake kikamilifu, jeshi la polisi lazima lifanye uchunguzi kwa haraka mara tu baada ya kupokea taarifa za* | Tunapendekeza kufumuliwa kwa mfumo wa taasisi za kiupelelezi hasa Jeshi la Polisi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | *uharifu. Mawakili wa serikali lazima wawe na uhakika wa ushahidi wanaopanga kuutumia kujenga kesi yao, wasije na tuhuma au fununu bila kuwa na uhakika kama fununu hizo zitamtia hatiani mtuhumiwa".* Rejea kiambatanisho Number, 8 | |
| 2. | **KUTOKANA UZOEFU ULIOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA ASASI YAKO, BAINISHA CHANGAMOTO ZILIZOPO KATIKA MFUMO WA HAKI JINAI ZIKIWEMO SERA, SHERIA, KANUNI, TARATIBU NA MIONGOZO NA NINI KIFANYIKE ILI KUONDOSHA CHANGAMOTO HIZO?** | | |
| | **Suala** | **Tatizo** | **Mapendekezo** |
| | Mamlaka ya Mwendesha Mashtaka wa Taifa kuingia *Nolle Prosequi* | Pamoja na kuwepo kwa mabadiliko ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985 juu ya zuio la mamlaka ya DPP hususani kumrudisha mtuhumiwa aliyeachiwa kwa Nolle Prosequi tena mahakamani<br><br>Bado kumekuwa na hitaji la kuhusisha mahakama katika mwenendo wa matumizi ya mamlaka ya DPP. | Ili kulinda haki za mtuhumiwa na kudhibiti mamlaka ya DPP kwa kuhusisha mahakama baada ya DPP kuwasilisha ombi la ridhaa ya kuingia Nolle Prosequi.<br>Mathalani nchini Kenya<br>Maamuzi ya Mahakama Kuu katika kesi ya Bwana **Cripus Karanja Njogu v. AG**<br>Iliamua kuwa DPP atahitajika kuomba ridhaa ya mahakama kabla ya kuingia *Nolle Prosequi.* |
| | Dhamana | Kuna baadhi ya makosa yalioorodheshwa katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai hayana dhamana hivyo basi mhusika hukaa rumande/mahabusu kwa muda | Haki ya dhamana iwe kwa makosa yote ili tuweze kulinda haki ya usawa mbele ya sheria kwa mujibu wa Ibara ya 13(6)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,1977. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | mrefu kwa kigezo cha upelelezi kutokamilika kabla ya shtaka lake kupelekwa mahakamani. Na pia mshtakiwa huyo muda mwingine hakutwi na hatia yoyote kwenye hilo shtaka, hivyo mshukiwa hupoteza muda mwingi akiwa rumande na pia shauri lake litakapoitwa mahakamani. | Rejea Ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kuhusu Makosa yasiyokuwa na Dhamana. |
| **3.** | **MAPUNGUFU NA CHANGAMOTO ZILIZOPO KATIKA SHERIA** | | |
| i. | **SHERIA YA KUPAMBANA NA MADAWA YA KULEVYA** | | |
| 1 | Kifungu cha 32 | Kifungu cha 32 cha sheria hii kilifanyiwa marekebisho na kifungu **cha 12 na 13 cha Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali No. 7 2022** kilichoipa mamlaka ya madawa ya kulevya pamoja na maafisa wake, mamlaka ya kiPolisi ikiwemo ukamataji na upekuzi.<br><br>Mbali na mabadiliko hayo, kifungu hiki pia kiliongeza wigo wa maafisa wa mamlaka wakati wakitekeleza majukumu yake kwamba watatekeleza majukumu yao kana kwamba ni maafisa wa Jeshi la Polisi hii imepewa mamlaka mpaka ya kuchukua maelezo ya onyo pamoja na *statement*. | Kituo kinapendekeza kufutwa kwa kifungu hiki kwa hoja kwamba jukumu la mamlaka libaki kama ilivyo katika kifungu cha 4 cha sheria na jukumu la ukamataji na upekuzi libaki kwa jeshi la Polisi kitengo cha madawa ya kulevya.<br><br>Hii ni kutokana na ukweli kwamba maafsa wa mamlaka hawana mafunzo au taaluma ya mambo ya upelelezi ikiwemo uchukuaji wa maelezo ya onyo.<br><br>Badala yake mamlaka ibaki na jukumu la kiutaalam na la kubaini *(intelijensia)* mbinu za ovu zinazotumika kuingiza na kusambaza madawa ya kulevya nchini. Aidha, kuendelea kujenga uwezo kwa wananchi na jamii kiujumla kuhusu athari za madawa ya kulevya. |

| | SHERIA YA MWENDENO WA MASHAURI YA JINAI SURA YA 20, | | |
|---|---|---|---|
| | Private Prosecution<br>Kifungu cha 99 | Mamala ya DPP kuingilia mchakato wa Private Prosecutor baada ya kupewa ruhusa na mahakama.<br><br>Hii inanyima haki kwa mtu ambaye hana imani na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kupata nafuu ya kisheria kwa kwenda kushtaki. | Kurekebisha sheria ili kuondoa sharti la kibali cha DPP. |
| | **Kifungu cha 37** | Mfumo dhaifu wa utoaji wa fidia kwa wahanga wa makosa ya jinai wakati wanasaidia uhalirifu usitokee kwa maafsa wa mahakama<br><br>Licha ya kifungu hiki kuwepo kwa mda mrefu lakini bado kimekuwa na changamoto za utekelezaji wake kwa mujibu wa ibara ya 107A(2) ( c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na kutokuwa na sheria ya utekelezaji wake mpaka sasa | Tunapendekeza kutungwa kwa sheria itakayoratibu masuala ya fidia katika katika jinai kwa mujibu wa ibara ya 107A(2) ( c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 ili kusaidia wahanga wa wanaopata majeraha au kufariki wakati wakisaidia uharifu usitokee kwa maafsa wa mahakama. |
| | **Kifungu cha 348**<br>Mfumo wa dhaifu wa mahakama kutoa fidia kwa wahanga wa makosa ya jinai | Kifungu cha 348 cha sheria hii kinatoa haki ya jumla ya wahanga wa uharifu wa kijinai kuomba fidia baada ya mtuhumiwa kutiwa hatiani, hata hivyo kifungu hiki | Tunapendekeza kutungwa kwa sheria itakayowezesha kutumika kwa kifungu hiki kwa mjibu wa ibara ya 107A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kinaonekana kuwa na masharti ambayo hayawezi kutekelezeka<br><br>Kuthibitisha hoja hii, tunaialika tume ijiongoze katika kesi zifuatazo, ambazo mahakama za chini zilitoa fidia kwa wahanga wa kijinai lakini mahakama za juu zikatupilia mbali madai hayo kwa hoja kwamba wahanga hao wangefungua madai hayo katika kesi za madai<br>***1. Jamhuri dhidi ya Tilusubya Mwishaki na wengine (1984) TZHC 30 [10 August 1984] au 1983 TLR 422(TZHC)***<br>***2. Jamhuri dhidhi ya Abel Rajab Marejeo ya Jinai No. 6 ya mwaka 2022 Mahakama kuu ya Tannzania masijala ya Dodoma***<br>***3. Abdulla Tifu Leonard dhidi ya Jamhuri Rufaa ya Jinai No. 73 ya Mwaka 2021, Mahakama kuu ya Tanzania masijala ya Bukoba*** | |
| | **Kifungu cha 14 (2)** Ukamataji unaofanywa na Afisa wa Polisi | Mamlaka ya kumuweka chini ya ulinzi mshukiwa wa uhalifu kwa muda wowote kabla ya kumfikisha mahakamani ikiwa **ofisa wa Polisi anayehusika na upelelezi anaona inafaa** kulingana na mazingira | Ni vema kuweka ukomo wa mtu kushikiliwa, kwa kulazimisha kifungu hiki kiendane na **kifungu cha 50, 51 na 64 cha Sheria hii.**<br><br>Pia, kuunganisha kifungu cha 14 na Kifungu cha 30 ili kuleta mantiki wakati utekelezaji au tafsiri ya sheria |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | yaliyopo wakati upelelezi ukiendelea.<br><br>Hakuna ukomo wa Polisi kumshikilia mtuhumiwa aliyemkamata, kifungu hiki hutumika vibaya kwa watu kuwekwa chini ya ulinzi wa polisi Polisi kufikishwa mahakamani kwa msingi wa kifungu hiki.<br><br>Kifungu hiki kinaweka mazingira ya rushwa. | |
| | **Kifungu cha 16 na 31**<br>Ukamataji unaoweza kufanywa na mtu binafsi | Changamoto ya kifungu hiki hakitoi ufafanuzi nini kinachotakiwa kufanyika baada ya mtu binafsi kufanya ukamataji. | Kifungu hiki kiunganishwe na kifungu cha 31 kinachoeleza nini kifanyike baada ya mtu binafsi kukamata ili kuweka mantiki ya kifungu cha 16.<br><br>Maboresho ya kifungu cha 31 yaanishe muda maalum angalau si zaidi ya saa moja (1) mkamataji kumfikisha mtuhumiwa Kituo cha Polisi cha karibu au ikiwa kituo kipo mbali, ampekeleke wa mtendaji wa Kijiji au mtaa wakati wanafanya jitihada za kuwasiliana na Polisi au kumfikisha Kituo cha Polisi. |
| | **Kifungu cha 54 (2)**<br>Haki ya Kuwasiliana na Mwanasheria, Rafiki au Ndugu | Kipengele hiki kinaweka mamlaka kwa Afisa wa Polisi kukataa haki ya mtuhumiwa aliye chini ya kizuizi kuwasiliana na mwanasheria, rafiki au ndugu kwa lengo la kuzuia mazingira ya kuharibika kwa ushahidi. | Kifungu hiki kifutwe<br><br>Msingi:<br>Ibara ya 14 ya Mkataba wa Haki za Kiraia na Kisiasa, 1966. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **Kifungu cha 11 12 na 21** Matumizi ya nguvu wakati wa ukamataji | Kifungu hiki kimeleta changamoto ya matumizi ya nguvu kubwa yaliyopelekea maumivu makubwa pamoja na vifo wakati wa ukamataji. | Kufanya marekebisho ya kifungu hiki, kufafanua kwa kuweka viwango vya mtumizi ya nguvu. Ikiwemo, kuweka zuio la matumizi ya silaha za moto ikiwa mtuhumiwa hana silaha ya mto, pia, zuia shambulio kwa mtuhumiwa wakati wa ukamataji ikiwa yeye hajafanya shambulio lolote. |
| | **Kifungu cha 22** Kinga ya mtu binafsi | Mtu binafsi anayekamata analindwa kisheria ikitokea mtuhumiwa atakutwa huru na mahakama. Bahati mbaya kifungu hiki hakijaweka udhiibti na kumlinda mtuhumiwa dhidi ya ukamataji holela. | Kurekebisha sheria kuweka kosa kwa mkamataji ikiwa itathibitikiwa kuwa ukamataji wake haukuwa na nia njema. |
| | **Kifungu cha 26** Upekekuzi kwa Mwanamke | Kumekuwa na changamoto ya kutotekelezwa kwa kifungu hiki.<br>4. Ukamataji na upekuzi kwa wanwake uzingatie sheria. | Tunapendekeza kuweka adhabu endapo kifungu hiki kitakiukwa.<br><br>Hii ni kulinda haki na utu waa wanawake |
| ii. | **SHERIA YA UHUJUMU UCHUMI NA UHALIFU WA KUPANGWA SURA YA 200,** | | |
| 1. | Tafsiri ya neno Prosecutor | Maana ya neno *"Prosecution officer"* halina maana tena kuwepo kwenye sheria hii kwakuwa kifungu kinachotoa maana ya neno hilo (kifungu 27) kimefutwa. | Kurekebisha kifungu hiki kuruhusu mtu binafsi kushtaki.<br><br>Msingi: Kuhakikisha *fair trial chini cha Ibara 14 ya Mkataba wa Haki za Kiraia na Kisiasa, 1966.* |
| 2. | Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashataka kuipa | Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ya kuipa uwezo mahakama yoyote chini ya | Kufuta kufungu hiki ili na kuondoa mamlaka ya kwa DPP na kuacha mamlaka ya kuongeza |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | mamlaka mahakama za chini. | Mahakama Kuu kusikiliza kesi ya uhujumu uchumi.<br>Pamoja na ukweli kwamba **Kifungu cha 12** kinampa uwezo DPP kufanya hivyo bado tunaona changamoto inayoweza kutokea pale ambapo DPP akiamua kutumia utashi wake na mamlaka yake kuacha kwa makusudi mamlaka husika iliyoanzishwa na kupewa uwezo maalamu wa kusikiliza kesi za uhujumu uchumi na kukimbilia mahakama za chini ambazo pengine hazina pengine uwezo huo. | wigo wa mamlaka za kusikiliza mashauri kwa Muhimili wa Makama. |
| 3. | Kifungu cha 17<br>Wasajili na Manaibu wasajili kutuma ripoti kwa Waziri. | Kuweka masharti la Msajili wa Mahakama Kuu na Manaibu wa Wasajili wa Mahakama kutuma taarifa za makosa ya uhujumu uchumi kila baada ya miezi sita, pamoja na mwenendo wa watumishi wa umma waliyokutwa na makosa ya uhujumu uchumi kwa Waziri husika.<br>1. Kifungu hiki, kinaingilia Muhimili wa Mahakama kinyume na ibara 107A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,1977.<br>2. Ni jukumu la kila muajiri kujua au kuwa na taarifa za waajiriwa wake wote kuhusu mienendo badala ya kuweka sheria ya kuwataka | Kifungu kifutwe.<br><br>Jukumu la kutuma taarifa zielekezwe kwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Wasajili na Manaibu kulazimika kutuma ripoti kwa Waziri. | |
| 4. | Kifungu cha 24 (4) na 24(6) | 1. Kifungu cha 24 (4) kinatoa siku ishirini na moja (21) tu kwa Inspekta Jenerali wa Polisi za kuwasilisha mali za mtuhumiwa mahakamani kwa ajili ya kutaifaishwa au kama itakavyoelekezwa ikiwa mtuhumiwa amekimbia au kutoonekana.<br><br>2.Kipengele hiki kinakinzana na kifungu cha 5 cha Sheria ya Proceeds of Crimes inayotoa maana ya *"absconding"* ikimaanisha mazingira ya mtu kutoonekana ndani ya miezi sita (6).<br><br>3.Hivyo, IGP kupewa mamlaka ya kuingia na kuchukua na kutumia atakavyoona inafaa mali aliyokuwa inamilikiwa au kusimamiwa na *"absconded person"* baada ya siku 21 kuisha na kupata kibali cha mahakama si sawa kwa kuwa inaweka nafasi ya matumizi mabaya ya mali za watu na kupotea pasipo majibu.<br><br>4.Pia, kifungu 24(6) kinazuia haki ya *"absconded person"*ikitokea | Utaratibu wa kutaifa au kuharibu mali ya mtuhumiwa aliyekimbia/aliyejificha au asiyepatikana bila kujulikana alipo ndani ya siku 21 na kumpa mamlaka IGP baada ya mahakama kutoa maamuzi chini ya kifungu cha 23(3), anaweza kutaifisha.<br><br>Utaratibu wa kushughulika na mali za mtu alikimbia/kupotea baada ya mahakama kutoa maamuzi uendane sambamba chini ya *Sheria ya Proceeds of Crimes.* |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | amerudi au ameonekana kudai mali yake iliyochukuliwa. | |
| 5. | Kifungu cha 25 (1) Kukasimisha mamlaka ya DPP | Kifungu hiki akiendani na msingi uliyowekwa kwenye kifungu cha 23 cha sheria mama ya Taifa ya Huduma ya Mashataka, *The National Prosecutions Service Act (NPSA), Sura Na. 420* ambacho kimeweka msingi wa mamlaka ya DPP kukasimisha madaraka yake kwa mtumishi yoyote chini ya sheria ya NPSA au public prosecutor.<br><br>Badala yake Sheria ya Uhujumi Uchumi imempa mamlaka ya kumkasimisha mtumishi yoyote wa umma. | Ni vema kwenye suala la Mamlaka ya DPP kusimamiwa au kuongozwa na sheria ya *National Prosecutions Service Act Cap 430.* |
| 6. | Kifungu cha 36 (2)(3) | Mamlaka ya DPP kuzuia dhamana,<br><br>Kwa kurejea maamuzi ya Mahakama Kuu katika kesi ya Jeremiah Mtobesya dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambayo ilitangaza kuwa kifungu cha 148(4) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985 kuwa kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. | Tunapendekeza zuio la dhamana kuongozwa zaidi na mahakama, kwa kuipa mahakama mamlaka ya kupokea na kusikiliza maombi ya dhamana badala ya kuacha mamlaka kwa DPP kuweka hati ya kuzuia dhamana bila mahakama kusikiliza ombi hilo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Kwa kutumia Kanuni ya *Statute in Pari materia* kifungu cha 36 (2)(3) cha Sheria ya Uhujumu Uchumi pia tunapendekeza kifutwa kwa kulinda maslahi ya mtuhumiwa, pia kwenda sambamba na dhana ya mtu kuwa hana hatia *"Presumption of Innocence"*. | |
| 7. | Kifungu cha 44<br>*Alternative Verdict*<br><br>"Hukumu mbadala" | Kifungu hiki kinaweka mamlaka kumtia mtu hatiani kwa kosa ambalo hata kama hakushitakiwa nalo.<br>Hii ni kinyume na principle ya "fair trial" | Kifungu hiki kifutwe |
| 8. | Kifungu cha 47 (3) c<br><br>Haki ya Kusikilizwa; | Sheria imeweka mazingira ambayo mtu hatopewa haki za kusikilizwa ikiwa atakuwa –*disruptive*.<br>Neno disruptive linaweza kutafsiri wa njia mbalimbali ni neno lenye utata wa kitafsiri. | Tafsiri ya disruptive iwekwe bayana ndani ya sheria<br><br><br>Msingi: Ibara ya 16(3) a ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. |
| 9. | Kifungu cha 60 (11) | Sheria imeweka mamlaka yanayotekelezwa na Kamishna wa Forodha kutekelezwa na Inspekta Jenerali wa Polisi. | Kutenganisha majukumu, majukumu ya Kamishna wa Forodha baki kuwa mhusika mkuu na jukumu la ufilisi liongozwe na Sheria ya *Proceeds fo Crimes Act*. |
| **iii.** | **SHERIA YA KUDHIBITI UTAKATISHAJI WA FEDHA HARAMU, SURA YA 423** | | |
| | Kuhukumiwa mara mbili kwa mtuhumiwa wa | Kifungu cha 12 cha sheria hii kilifanyiwa marekebisho na kifungu | Kituo kinapendekeza kufanyiwa marekebisho kwa kifungu hiki ili kuondoa uwezekanao wa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | makosa ya uhujumu uchumi | cha 9 cha nyongeza ya mabadiliko ya sheria ya utakatishaji fedha Haramu No. 2 ya 2022 kilichoweka takwa la kosa la utakatishaji wa fedha haramu kuwa kosa linalojitegemea tofauti na awali ambapo kosa la utakatishaji wa fedha haramu lilitokana na kifungu cha 12, 57, 60 na nyongeza ya orodha ya uhumu uchumi iliyoko katika sheria ya uhujumu uchumi.<br><br>Kwa mjibu wa kifungu cha 12(4) cha sheria hii mtuhumiwa aliyekuhumiwa kwa kosa la utakatishaji fedha kwa mjibu wa kifungu cha 12(1), anaweza kuhukumiwa tena kwa kosa hilohilo kwa mjibu wa kifungu cha 12, 57, 60 na nyongeza ya orodha ya makosa uhujumu uchumi chini ya sheria ya uhujumu uchumi. | watuhumiwa wa makosa ya utakatishaji wa fedha haramu kuhukumiwa mara mbili kwa kosa moja kinyume na kanuni za kijinai.<br><br>Tunapendekeza kifungu kibaki kama kilivyokuwa hapo awali. |
| | Uwepo wa Predicate Offences | Ongezeko la idadi kubwa ya makosa tangulizi (predicate offences) katika Sheri ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu, kifungu cha 3, imepelekea makosa ya kawaida kuwa utakatishaji fedha/uhujumu uchumi. | Kurekebisha Sheria ya Uhujumu Uchumi ili kupunguza idadi kubwa ya makosa tangulizi yaliyoletwa mwaka 2016. |
| iv. | **SHERIA YA UTAWALA WA MAHAKAMA NA.2, 2011** | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **Kifungu cha 50 na 51**<br><br>Kamati za Maadili za Maafisa wa Mahakama za Mkoa na Wilaya. | 1. Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwa wenyeviti wa kamati za maadili za mahakimu kwenye mkoa au wilaya husika<br><br>2.Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya kuwa sehemu ya kamati hiyo.<br>3. Mamlaka ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya kualika/kuongeza wajumbe wawili katika kamati hiyo. | Tunapendekeza marekebisho kwa kufuta kifungu hiki ili kuondoa sehemu ya muhimili mmoja kuingia au kufanya maamuzi katika muhimili mwingine.<br><br>Jukumu la kusimamia maadili libaki kwa viongozi wa mahakama pekee. Kwa kuwa mahakama inautaratibu mzuri na uzoefu wa kusimamia maadili wa watumishi wake.<br><br>Ili kuendana na dhana ya mgawanyo wa madaraka na uhuru wa mihimili ya dola kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. |
| VII. | **SHERIA YA KUCHUNGUZA VIFO NO. 17 YA MWAKA 1980** | | |
| | Sheria hii ina udhaifu hasa kwenye eneo la uchunguzi wa vifo venye utata | Hivi karibuni kumekuwa na vifo vingi venye utata hasa katika vituo vyetu vya Polisi, licha ya Tanzania kuwa na sheria ya uchunguzi wa vifo**( The Enquest Act) lakini bado sheria hii inaonekana kutokuwa na mchango wowote hasa katika eneo la uchunguzi kutokana na sheria kutokuwa bayana juu ya mahakama yenye mamlaka kisheria ya kufanya uchunguzi huo** | Tunapendekeza<br>Mosi, kufumuliiwa kwa sheria hii ili uchunguzi wa vifo vyenye utata ufanywe na Mahakama kuu badala ya utaratibu wa sasa ambao sheria inataka ateuliwe Coroner<br><br>Pili tunapendekeza utaratibu wa kuwasilisha maombi mahakama kuu uwe kama utaratibu wa kuwasilisha maombi mengine yoyote hivi sasa<br><br>Tatu, Mahakama kuu kama itajiridhisha kwamba kulikuwa na uzembe katika kifo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | hicho basi iwe na mamlaka ya kupendekeza kwa Mkurugenzi wa mashitaka kuwachukulia hatua za kijinai wanaohuika na kifo hicho, na maamuzi mengine ambayo mahakama kuu itaona inafaa kutoa<br><br>Nne, mahakama kuu ipendekeze kwa mamlaka za nidhamu kama aliyehusika ni Polisi kwa mamlaka zake za nidhamu kumchukulia hatua za kinidhamu kwa mjibu wa sheria za kipolisiPolisi |
| VIII. | **SHERIA YA KUPAMBANA NA KUZUIA RUSHWA SURA YA 329 KAMA ILIVYOFANYIWA MAREJEO MWAKA 2022** | | |
| | Maoni ya Jumla | Kiuhalisia hii ndo sheria Mama yenye jukumu na dhamana ya kupambana na kuzuia rushwa nchini, changamoto kubwa ya taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa miaka ya hivi karibuni imekuwa ya kutia mashaka kutokana na taasisi hii kuanza kujishughulisha na majukumu ambayo kimsingi hayapo kwa mjibu wa sheria inayoianzisha taasisi hii.<br><br>Kwa mfano miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia taasisi hii yenye jukumu la kupambana na kuzuia rushwa ikijihusisha na kazi kama vile kukusanya madeni, kumiliki | i.<br><br>Tunapendekeza kuboreshwa mifumo ya kisera na kitaasisi ili kuirejesha TAKUKURU kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwa mjibu wa sheria. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | mahabusu ambazo kimsingi hazina vigezo vya kuwa mahabusu, kufanya kaguzi za ufanisi, kukagua miradi ya maendeleo na kadhalika. | |
| | | | |
| **A.** | **KWA MAONI YAKO, NINI KIFANYIKE KWENYE ENEO LA SERA, SHERIA, MIONGOZO NA MIUNDO ILI KUBORESHA MFUMO WA HAKI JINAI NCHINI?** | | |
| | | **1. Mauaji na ukatili chini ya mamlaka ya polisi**<br>Hivi karibuni kumeibuka mwenendo usio wa kawaida wa watuhumiwa kuawa wakiwa mikononi mwa huku sababu za vifo hivyo zikiwa zimejaa utata mkubwa. Kwa mfano, kisa cha mfugaji aliyefia<br>Kituo cha Polisiilivyoripotiwa katika Gazeti la Nipashe la tarehe *16 Mwezi Feburuari 2023* lilishapisha kichwa cha habari kisemacho ***Polisi; Ameja mahabusu kwa kutumia nguo yake ya ndani.***<br><br>2. Kesi za madai kuwa jinai<br><br>3. Mtu aliyemaliza kifungo au kuhusisha na kesi za ukatili dhidi ya watoto hasa wa kingono kutorudi kwenye mazingira au kazi ya aina hiyo hiyo ili kulinda watoto. | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Kufungamanisha ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na Sekta ya Ustawi wa Jamii | Kuboresha kwa kuimarisha mfumo wa usalama na ulinzi katika ngazi mtaa.<br><br>Kwa ushirikiano wa maafisa ustawi wa jamii. | Mifumo wa usalama na ulinzi ifungamane na mifumo ya ustawi wa jamii. Kwa kuwa, sekta ya ustawi wa jamii inawataalam wanaoweza kurekebisha tabia kwa njia maalum kutokana na taaluma yao |
| | Kutunga Sera maalumu ya Haki Jinai | Hakuna Sera moja ya haki jinai inayoongoza mfumo mzima wa haki jinai. | Kutunga sera na mpango wa utekelezaji wa Sera ya Haki Jinai Nchini. |
| | Kuruhusu mfumo wa wapelelezi binafsi | Itaimarisha ulinzi wa haki za watuhumiwa na waathirika wa matukio ya uhalifu ambao hawana imani na Ofisi ya Mashtaka.<br><br><br>Sh | Kutunga sheria itakayoongoza usajili, usimamizi na mwenendo wa wapelelezi binafsi |
| | Msongamano wa mahabusu magerezani kuliko wafungwa, ikiwemo watoto ambao hawatakiwa kuwemo magerezani. | Kwa mujibu wa gazeti la the citizen la tarehe 6 Feburuari 2019 siku ya jumatano, kwa mwaka 2018 gereza la Segerea lilikuwa na jumla ya mahabusu wa kiume 1723 ambapo kati yao ni mahabusu 158 pekee walitiwa hatiani na kuwa wafungwa, lakini pia gereza hilo lilikuwa na jumla ya wafungwa wa kike 313 ambapo kati yao ni 66 pekee ndo walitiwa hatiani. Gereza hilo pia lilikuwa na jumla ya mahabusu 1565 ambapo kati yao ni 247 pekee ndo walitiwa hatiani na kuwa wafungwa. | Tunapendekeza kuimarishwa kwa mfumo wa parole nchini.<br><br><br>Kutumia mfumo wa<br>Adhabu mbadala – mfano kifungo cha nje kwa makosa mepesi. Utaratibu uboreshwe, Mahakama iadopt mfumo huu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Hakuna Mpango wa Haki za Binadamu wa Taifa | Ni zaidi ya miaka miwili nchi haina mpango huo. | Kutungwa na utekelezaji wa mpango |
| | Kutekeleza mapendekezo ya Universal Periodic Review (UPR) | Mapendekezo mahususi ya kuboresha mfumo wa haki jinai, yaliyotolewa na Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu katika Duru ya 3 ya mwaka 2021. | Kutekeleza mapendekezo hayo |
| B. | **KWA KUMALIZIA, ENEO AU JAMBO GANI LA ZIADA UNAONA LINAWEZA KUSAIDIA TAASISI ZA HAKI JANAI KUONDOSHA MALALAMIKO YA WANANCHI AU WADAU NA KUHAKIKISHA HAYAJIRUDII?** | | |
| | | | |
| | Kutenganishwa kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya jinai ( DCI) | Kutoka kuwa sehemu ya Jeshi la Polisi ili kuongeza ufanisi na weledi wa kiupelelezi katika idara hii. Ni wazi kwamba, kesi nyingi zimekuwa zikionekana kuwa na udhaifu hasa katika eneo la ushahidi zinapokuwa mahakamani.<br><br>Hii itasaidia idara hii kuwa na watu wenye weledi na uelewa wa kutosha juu ya sayansi ya intelijensia ya uchunguzi.<br><br>Kuthibitisha hoja hii tunaialika tume ijiongoze katika kesi zifuatazo ambazo mahakama kuu na Mahakama ya Rufani kwa nyakati tofauti zilionesha waziwazi kuwepo kwa udhaifu na uelewa mdogo wa kiushaidi hivyo kupelekea | Kufanya marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Polisi Huduma Saidizi, Sura 322 kwa kuiondoa Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | mahakama ya rufani kubatilisha maamuzi ya mahakama za chini.<br><br>1. **Hosea Francis @Ngala &Maraia Hosea @Ulanga dhidi ya Jamhuri Rufaa Na. 408 2015 Mahakama ya Rifani masijala ya Dododma**<br>2. **Yusuph Aman Dhidi ya Jamhuri Rufaa Na. 255 mwaka 2015 Mahakama ya Rufani**<br>3. **Jamhuri dhidi ya Issa Mohamed@ Chiwele & Weingine Jinai Na. 39 2016 Makama kuu Lindi** | |
| | Kuanzishwa kwa chombo huru**( Independent Police Oversight Authority)** | Kuwe na chombo maalum kitakachoshughulika na malalamiko ya wananchi juu ya uvunjifu wa haki za binadamu ambao umekuwa ukifanywa mara kwa mara na Jeshi letu la Polisi. | Tunaialika tume kujiongoza katika kiambatanisho Namba 2 ambacho ni Muswada wa Mfano ( Model Bill) ambao kituo kimeandaa kama mbadala ambao tume kama itaona inafaa yaweza uchukua. |
| | Kuongeza ushirikiano na taasisi za Elimu ya Juu katika kufanya maboresho ya sera, mitaala na miongozo ya Jeshi la Polisi. | Kutokana na changamoto mbalimbali zilizoainishwa katika uchambuzi huu zinachangiwa sababu za kisera ikiwemo mifumo ya kisera na kukosekana kwa umahiri unaoendena na mabdiliko ya Sayansi na Teknolojia. | Kufumuliwa kwa mitaala ya Jeshi la Polisi ili kuongeza mitaala inayohusu Sayansi ya jinai na Intelijensia ya uchunguzi na upelelezi ili kuongeza ufanisi wa maafsa wetu wa upelelezi tofauti na hali ya sasa, au tunapendekeza kuanzishwa kwa shahada ya sayansi ya jinai, uchunguzi, upelelezi na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Ni muhimu kushirikiana na Taasisi za Elimu ya Juu katika kupita mifumo na kutengeneza mitaala ya elimu pamoja na kozi maalum zitakazoziba pengo hilo. | intelijensia ya jinai itakayokuwa inatolewa maalum kwa maafsa wetu wa upelelezi baada ya kutoka katika mafunzo ya awali ya uaskari. |
| | | | |
| | Dhamana kwa makosa yote ya jinai kwa **masharti yatakayowekwa na Mahakama** | Kuweka masharti maalum yatakayo ongoza mahakama namna ya kutoa dhamana katika makosa yasiyokuwa na dhamana kama ilivyo amuriwa katika Kesi ya *Republic V Lucy Njeri Waweru & 3 Others, Nairobi Criminal Case No. 6 of 2013,*<br><br>*the court listed some of the factors as being:*<br><br>*a. Whether the accused persons were likely to turn up for trial should they be granted bail,*<br><br>*b. Whether the accused persons were likely to interfere with witnesses,*<br><br>*c. The nature of the charges,*<br><br>*d. The severity of the sentence,* | Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985 irekebishwe ili kutimiza dhana ya mtu kutokuwa na hatia kama ilivyoainishwa katika *Ibara ya 13 (6) (b)ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.* |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | *e. The security of the accused if released on bond, and*<br>*f. Whether the accused person has a fixed abode within the jurisdiction of the court,*<br><br>*g. accused's previous criminal record,*<br><br>*h. detention of the accused person for his or her own protection,*<br><br>*i. the probability of the accused person tampering with evidence, and,*<br><br>*j. the strength of the evidence.* | |
| | Unafuu wa masharti ya dhamana – wadhamini ama mali, | Changamoto ya watu kukosa dhama kwa masharti magumu yasiyokuwa na mfanano kati ya Kituo cha Polisi kimoja na kingine.<br><br>Watuhumiwa wengine huambiwa lazima waleta mdhamini ambaye ni mfanyakazi katika Utumishi wa Umma. | Masharti yawe nafuu, yaendane na uhalisia wa maisha ya mtu;<br><br>Watuhumiwa wajidhamini kwa kutumia taarifa zao rasmi kama NIDA |
| | Upangwaji wa vikao (sessions) Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani | Kumekuwa na changamoto ya vikao kupangwa | Kuongeza matumizi ya teknolojia katika kusikiliza kesi za Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Zoezi la upekuzi magerezani | Jeshi la Magereza lizuiwe kufanya zoezi la upekuzi kwa mateso, ikiwemo kuwavua nguo mahabusu na wafungwa/ | Kwa kuridhia *Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Mateso, Ukatili, na Mambo yanayotweza Utu wa Binadamu, 1984* |
| | Lishe, huduma za afya na usafi magerezani | Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuhusu jambo hili. Hali hii inawaathiri wanawake zaidi kwani kutokana na maumbile yao huathirika kiafya. | Kuendana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa wafungwa yaani;<br><br>*The United Nations Standard Minimum Rules for the Treatment of Prisoners.* |
| | | | |
| | | | |
| | Mawasiliano ya ndugu wa mtuhumiwa | Kumekuwa na changamoto ya namna ya mawasiliano magerezani . Namna ya jinsi ya kuwasiliana si ya kiutu. | Tunapendekeza kuweka mfumo bora wa mawasiliano kati ya ndugu na mtuhumiwa au mfungwa tofauti na utaratibu wa sasa. |
| | Upatikanaji wa taarifa mbalimbali za mifumo ya haki jinai. | Ni changamoto kupata taarifa ya idadi ya jumla ya kesi zilizoisha, zinazoendelea pamoja na taarifa mbalimbali katika mfumo wa haki jinai. | Tunashauri taarifa hizo ziwekwe kwenye tovuti za taasisi husika pamoja na mitandao ya kijamii ya taasisi hizo ili kuweka urahisi wa upatikanaji wa taarifa. |
| | | | |
| | Msaada wa kisheria magerezani | Pamoja na kuwepo kwa Sheria ya Msaada wa Sheria, 2017 inayoweka haki za wafungwa kupata msaada | Tunapendekeza Tume itoe wito kwa Magereza kuharakisha mchakato wa kutoa vibali hiyo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | wa kisheria, bado kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa vibali hivyo. Huchukua hadi mwezi mmoja kupata kibali hicho. | |
| | Kesi za Wahamiaji na Wakimbizi | Kesi za uhamiaji – Polisi wajengewe uwezo wa kutenganisha wahamiaji haramu na wanaokimbia kadhia mf: raia wa Burundi, Ethiopia, badala ya kuwafunga gerezani na kuwahudumia, ni nafuu zaidi kuwarudisha kwao ama kuwakabidhi kwa mamlaka kama UNHCR/IOM ikiwa wana sifa | Ili kuendana na Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Wakimbizi. |
| | | Kuhamishwa kwa wafungwa kutoka gereza moja kwenda gereza la mkoa mwingine, ambapo rufaa ya muhusika haijafunguliwa. | |
| | | | |
| | **Kuweka mkakati endelevu wa matumizi ya teknolojia katika sehemu za umma** Kituo kinapendekeza kuwepo kwa mkakati wa kuweka hitaji la kuwa na kamera za usalama katika maeneo mbalimbali. Kwa kuanzia, kuongeza | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | msisitizo wa kufungwa kwa kamera katika majengo mbalimbali ya umma na binafsi, pia kuwa na mpango wa muda mrefu wa kiserikali wa kufunga kamera za ulinzi. Pendekezo hili linatambua ufinyu wa bajeti, lakini kuwa na mpango endelevu utasaidia kutekeleza jambo hilo kwa awamu. | | |